**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**634** **STADI ZA KAZI**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2019**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila Sehemu **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika upambaji wa nguo kwa kutumia rangi.
2. Onesha umuhimu wa upimaji katika somo la Stadi za Kazi kwa kutumia hoja nne.
3. Bainisha faida nne za kutumia vifaa vya asili katika ususi.
4. Taja mambo manne ya kuzingatia katika kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.
5. Orodhesha tahadhari nne za kuchukua wakati wa mazoezi ya kuimba.
6. Eleza upungufu wa kutumia njia ya mhadhara kufundishia mada ya "Ushoni wa nguo".
7. Taja madhara manne yanayoweza kutokea endapo kanuni za usafi na usalama wa chumba cha kupikia hazitazingatiwa.
8. Eleza kwa kifupi mbinu nne zinazoweza kutumika kufundishia na kujifunzia dhana ya "Uimbaji wa solfa".
9. Taja faida nne atakazozipata mwanafunzi kwa kujifunza fani ya utengenezaji wa mapambo mbalimbali.
10. Bainisha hasara nne zinazoweza kujitokeza iwapo mbinu ya majadiliano haitaandaliwa ipasavyo katika kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **Mawili** katika sehemu hii.

11. Fafanua fani sita zinazopatikana katika sanaa za maonyesho.
12. Chambua aina tano za mishono ya kutumia mikono na uoneshe kazi ya kila mshono.
13. Eleza faida sita za kufuga wanyama.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **Mawili** katika sehemu hii.

14. Eleza umuhimu wa msingi wa utendaji, umakini na udadisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa kutumia hoja tano.
15. Chambua hatua tano za kufanya tathmini ya somo la Stadi za Kazi.
16. Onesha umuhimu wa mbinu ya ziara katika kufundishia mada ndogo ya "Matengenezo ya baiskeli" kwa kutumia hoja sita.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org